BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Sita – Tarehe 19 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

100. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Ni athari gani za kiafya na kimazingira zinazoweza kupatikana kutokana na kuwepo kwa masalia ya takataka kwenye fukwe zetu.

**<u>Ofisi ya Rais Ikulu:</u>**

170. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:

(a) Je, ni taasisi ngapi na zipi ambazo kwa sasa zinaendeshwa kwa mfumo wa TEHAMA.

(b) Je, ni kwa kiasi gani mashirika na taasisi hizo zinalinda na kuweka uwazi pamoja na udhibiti wa mifumo na data za TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yao.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

96. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha Idara ya Msaada wa Kisheria hapa nchini.

Je, ni maeneo gani ambayo yamekuwa na changamoto kubwa linapokuja suala zima la msaada wa kisheria kwa wananchi wetu.

108. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ni kwa kiasi gani Mahakama za Zanzibar zimeimarika vyema katika mambo mbali mbali kwenye Awamu hii ya Nane.

**<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>**

18. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kiasi gani mashirikiano na mahusiano kati ya Sekta binafsi na Serikali yanaimarika.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

15. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kada ya Ununuzi ni moja ya sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na umuhimu wa kada hii, bado inakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo kukosekana kwa kanzi data ya wataalamu wa manunuzi na upungufu wa maslahi kwa watumishi wa kada hii.

    (a) Je, ufahamu wa Serikali yetu uko vipi juu ya changamoto zinazoikabili kada hii.

    (b) Kwa mujibu wa kanzi data, ni watumishi wangapi wa fani ya Ununuzi wameajiriwa Zanzibar na katika madaraja gani.

    (c) Serikali ina mkakati upi wa kutathmini upya maslahi ya watumishi wa fani ya ununuzi ili kuwaongezea motisha ya kufanya kazi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

142. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Uhaba wa maji safi na salama hupelekea tatizo la magonjwa ya matumbo na "typhoid".

    Je, ni kwa kiasi gani uboreshaji wa miundombinu mipya ya maji unachochea kupungua kwa idadi ya wagonjwa wa matumbo na "typhoid".

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

60. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Kukuwa kwa kasi kwa sekta ya michezo nchini kunaambatana na uhitaji mkubwa wa vifaa vya michezo.

    Ni lini Wizara itafikiria kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika viwanda vya kutengenezea vifaa vya michezo, ili kupunguza gharama kubwa ya kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

11. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Bungo ni moja ya tunda linalopatikana kwa wingi katika kisiwa cha Pemba na limekuwa zao muhimu kwa wananchi, hasa vijana wanaojipatia kipato kwa kuziuzia hoteli za kitalii na wafanyabiashara. Licha ya umuhimu wake, bungo ni zao lililosahaulika na linalopotea kwa kasi.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya tafiti kuhusu zao la bungo.

(b) Tathmini inaonesha nini juu ya uzalishaji wa bungo kwa mwaka na kiasi gani wananchi huingiza kwa biashara hii.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la bungo ili kuimarisha kipato cha wananchi.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto:

(a) Wizara ya Maendeleo ya Jamii ina utaratibu gani wa kujadiliana na wadau wa masuala ya ustawi wa jamii katika kupunguza changamoto za utoaji wa huduma za ustawi wa jamii.

(b) Huduma za ustawi wa jamii hutolewa kwa utaratibu gani kwa lengo la kuzuia na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii kiakili, kimwili, kimaadili hasa kwa makundi maalumu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

90. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya namna gani ya kuongeza pato linalotokana na utalii na kuzuia zaidi mianya ya upotevu wa mapato yanayotokana na sekta ya utalii.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

139. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa maendeleo ya elimu pamoja na mambo mengine, yanategemea uwiano sawa baina ya walimu, vifaa na vitabu vya kufundishia wanafunzi wetu.

(a) Je, tathmini ipo vipi juu ya idadi ya walimu na vifaa vya kufundishia.

(b) Je, kwa kiasi gani tathmini hiyo inachochea na kukwaza ustawi wa mpango wa mageuzi ya kielimu.

(c) Je, tathmini iko vipi juu ya uwiano wa vitabu vya kiada na mahitaji stahiki ya wanafunzi wetu.

151. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la ufaulu katika skuli zetu pamoja na ongezeko la udahili wa vyuoni ambapo kunachangia sana ongezeko la uhaba wa ajira.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupambana na changamoto hii.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

76. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara zilizojengwa kwa kifusi katika jimbo la Paje, zimeshachimbika kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi tatizo hilo.

(b) Ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami.

(c) Je, Wizara yako inawaeleza nini wananchi wa Paje kuhusu tatizo hilo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

144. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Haiba ya mji wowote ule duniani unatambulika kutokana na usanifu wa majengo ya kisasa na yenye mvuto.

(a) Je, ni upi mpango mkakati wa kuzijenga nyumba za kisasa za makaazi katika maeneo ya Kilimani, Kikwajuni na Michenzani.

(b) Je, kwa namna gani Serikali itakamilisha mpango huo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kiasi gani kuimarika kwa Sekta ya Ujenzi katika ujenzi wa miradi mbali mbali ya kimkakati nchini, kunasaidia kukuwa na kuimarika kwa sekta ya biashara kwa wafanyabishara wa ndani wanaojihusisha na vifaa vya ujenzi.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**19 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**